



MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

TAARIFA KWA UMMA USAILI WA AJIRA

Dar es Salaam, 21 Machi, 2025

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilitangaza nafasi za kazi **1,596** katika fani mbalimbali kuanzia tarehe 06 hadi 19 Februari, 2025, ambapo maombi ya kazi **135,027** yalipokelewa.

TRA imepitia kwa umakini mkubwa maombi yote yaliyopokelewa na kupata waomba kazi **112,952** waliokidhi vigezo vilivyowekwa na hivyo kustahili kuitwa kwenye usaili wa mchujo wa kuandika (**Written Interview**) ambao unatarajiwa kufanyika kuanzia **tarehe 29 hadi 30 Machi, 2025**. Majina ya waliofanikiwa yatatangazwa kwenye tovuti ya TRA (www.tra.go.tz) tarehe **22/03/2025** na pia taarifa itatumwa moja kwa moja kwa kila muombaji kupitia barua pepe yake aliyotumia wakati wa kuomba kazi, Vilevile tarehe, mahali na muda wa usaili zimeonyeshwa kwenye wito huo.

Usaili wa Mchujo wa kuandika utafanyika katika Mikoa 9 kama ifuatavyo:-

1. Dar es Salaam ambayo itahusisha waombaji kutoka Dar es Salaam na Pwani;
2. Zanzibar ambayo itahusisha waombaji kutoka Unguja na Pemba;
3. Arusha ambayo itahusisha waombaji kutoka Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Tanga;
4. Dodoma ambayo itahusisha waombaji kutoka Morogoro, Dodoma, Singida, Iringa na Tabora;
5. Mtwara ambayo itahusisha waombaji kutoka Mtwara, Lindi na Ruvuma;
6. Mbeya ambayo itahusisha waombaji kutoka Mbeya, Songwe na Rukwa;
7. Mwanza ambayo itahusisha waombaji kutoka Mwanza, Shinyanga, Mara na Simiyu,
8. Kagera ambayo itahusisha waombaji kutoka Kagera na Geita; na
9. Kigoma ambayo itahusisha waombaji kutoka Kigoma na Katavi.

Utaratibu maalumu umeandaliwa kwa waomba kazi wenye mahitaji maalumu waliofanikiwa kuitwa kwenye usaili wa mchujo wa kuandika ili waweze kufanya usaili huo bila usumbufu.

Mchakato huu wa ajira utaendeshwa na Mshauri Mtaalam (**Consultant**) na Mamlaka itasimamia kwa karibu ili kuhakikisha haki inatendeka kwa waombaji wote. Aidha tunatoa wito kwa waombaji kazi wote kujiandaa vyema katika hatua zote za usaili ili kufanya vizuri katika mitihani hiyo na hatimaye kuajiriwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Waombaji watakaofaulu kwenye usaili wa mchujo wa kuandika wataitwa kwenye usaili wa mahojiano kwa tarehe, siku na mahali watakayotaarifiwa hapo baadae.

Kwa mawasiliano zaidi:

Piga simu bure: 0800 750 075 / 0800 780 078/0800110016

WhatsApp: 0744 23 33 33

Email: huduma@tra.go.tz / services@tra.go.tz

"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"

TRA

Imetolewa na:

MOSHI J. KABENGWE

Kny: KAMISHNA MKUU